TANGAZO LA SERIKALI NA. 909 la tarehe 22/12/2023

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU WA MADINI YA UJENZI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga,

chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazotolewa katika eneo la Halmashauri; na

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi, kampuni au asasi na Halmashauri kukusanya ushuru au ada kwa niaba ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Maombi ya kibali

4.-(1) Mtu anayekusudia kuanzisha machimbo ya madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwasilisha kwa Mkurugenzi maombi ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi ya kibali yatatakiwa kuambatishwa na taarifa zifuatazo:

(a) leseni ya uchimbaji wa madini iliyotolewa na Mamlaka husika;
(b) aina ya madini yanayokusudiwa kuchimbwa;
(c) umiliki pamoja na ukubwa wa eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi;
(d) mpango wa utunzaji wa mazingira katika eneo la machimbo; na
(e) muhtasari wa Mkutano wa Kijiji ambacho uchimbaji wa madini ya ujenzi utafanyika ukionesha kukubaliana na uchimbaji huo.

(3) Ndani ya muda wa siku saba tangu kupokea maombi, Mkurugenzi atatakiwa kukagua eneo ambalo uchimbaji wa madini ya ujenzi unakusudiwa kufanyika ili kujiridhisha iwapo eneo hilo linafaa kwa shughuli za

uchimbaji.

(4) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), baada ya kukamilika kwa ukaguzi wa eneo linaloombewa kibali, Mkurugenzi atatakiwa kukubali au kukataa maombi na endapo atakataa atatoa sababu za kukataliwa kwa maombi hayo.

Wajibu wa mpewa kibali

5. Mtu yeyote aliyepewa kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi atatakiwa:

(a) kulipa ada ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi ya kiasi cha shilingi laki tatu;

(b) kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hii na masharti ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi; na

(c) kulipa ada au ushuru utakaotozwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Muda wa uchimbaji na masharti ya usafirishaji

6.-(1) Shughuli za uchimbaji, uuzaji na ununuzi wa madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri zitafanyika kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni kila siku.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), Mkurugenzi anaweza kutoa kibali maalumu kuruhusu shughuli za uchimbaji, uuzaji na ununuzi wa madini ya ujenzi kufanyika nje ya muda ulioainishwa.

(3) Kila mmiliki wa gari linalosafirisha madini ya ujenzi atatakiwa kuhakikisha kuwa gari hilo limefunikwa wakati wote wa usafirishaji wa madini ya ujenzi.

Mamlaka ya afisa mwidhiniwa

7. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote yanapochimbwa madini ya ujenzi kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni kwa nia ya kufanya ukaguzi na kutoa ushauri wa uendeshaji wa shughuli za uchimbaji.

Ushuru wa madini ya ujenzi

8.-(1) Kila mnunuzi au msafirishaji wa madini ya ujenzi atatakiwa kulipia ushuru wa madini ya ujenzi kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Ushuru wa madini ya ujenzi utatozwa katika eneo la machimbo, barabara zinazoelekea au kutoka maeneo ya machimbo au eneo lolote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri.

(3) Mnunuzi yeyote atakayeshindwa kulipa ushuru anaotakiwa kulipa atatakiwa kupakua madini ya ujenzi kutoka katika chombo au kutochukua madini hayo mpaka hapo atakapolipa ushuru anaodaiwa.

Vituo vya ukaguzi

9.-(1) Kutakuwa na vituo vya ukaguzi wa malipo ya ushuru wa madini ya ujenzi katika njia zinazoingia au kutoka katika maeneo ya machimbo.

(2) Kila dereva wa chombo cha usafiri kilichobeba madini ya ujenzi atatakiwa kusimama katika kituo cha ukaguzi na kuonesha stakabadhi ya kielektroniki ili kuthibitisha kulipwa kwa ushuru wa madini ya ujenzi yaliyo katika chombo cha usafiri.

(3) Chombo cha usafiri kitakachokamatwa kwenye eneo la machimbo na dereva au mmiliki wake akakimbia au kutoroka, chombo hicho hakitaruhusiwa kutoka mpaka kitakapolipiwa faini na ushuru unaodaiwa.

Utoaji wa stakabadhi za malipo

10.-(1) Ada au ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au wakala ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(2) Utakuwa ni wajibu wa kila mlipa ada au ushuru kudai na kuhakiki stakabadhi ya malipo kulingana na kiasi cha fedha alicholipa.

(3) Utakuwa sio utetezi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, mtu kudai kuwa amelipa ada au ushuru lakini hakupewa stakabadhi ya kielektroniki.

Kufutwa au kusimamishwa kwa kibali

11.-(1) Halmashauri inaweza kufuta au kusimamisha kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi endapo itajiridhisha kuwa kuna ukiukwaji wa masharti ya Sheria Ndogo hii au masharti ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo ya (1), kabla ya kufuta au kusimamisha kibali, Halmashauri itatakiwa kutoa notisi ya siku saba ya kusudio la kufuta au kusimamisha kibali kwa mtu yeyote aliyepewa kibali cha uchimbaji.

(3) Notisi itakayotolewa kwa mujibu wa aya ndogo ya (2) itaainisha sababu za kufuta au kusimamisha kibali husika.

(4) Endapo kibali kitafutwa au kusimamishwa, mtu yeyote aliyepewa kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi atasimama kuchimba madini hayo.

Uteuzi wa wakala

12.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kwa ajili ya kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroni na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashuri.

Halmashauri kutowajibika kwa hasara

13. Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote atakayopata mnunuzi au msafirishaji wa madini ya ujenzi wakati wa kukusanya ushuru isipokuwa kama hasara

hiyo itasababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Makosa

14. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) ataanzisha machimbo ya madini ya ujenzi bila kuwa na kibali kilichotolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) atasafirisha madini ya ujenzi bila kulipa ushuru;
(c) atachimba madini ya ujenzi kabla au baada ya muda ulioruhusiwa kuchimba;
(d) atasafirisha madini ya ujenzi katika gari ambalo halijafunikwa;
(e) atamshawishi mtu au kundi la watu kutolipa ushuru;
(f) atakataa kutii agizo lolote atakalopewa na afisa mwidhiniwa wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;
(g) atakataa kulipa ushuru au kumzuia afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza wajibu wake;
(h) atakwepa kulipa ushuru kwa kupita njia tofauti na kituo cha ukaguzi;
(i) atachimba madini katika maeneo yasiyoidhinishwa;
(j) atachimba shimo kubwa kwa ajili ya madini na kuliacha bila kupanda miti au mimea mara baada ya madini hayo kumalizika; au
(k) atachimba madini bila kuwa na kibali cha uchimbaji.

Adhabu

15. Mtu atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi

kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha Kosa

16. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

---

JEDWALI LA KWANZA

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(1))*

KIBALI CHA UCHIMBAJI WA MADINI YA UJENZI

Kibali hiki kimetolewa kwa Bw/Bi: ……………………………………………….……wa S.L.P……………., Mlimba. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ameridhia Ndugu mtajwa hapo juu, aendeshe shughuli za kuchimba madini ya ujenzi katika eneo la …………………………Kijiji cha………………………. kata ya …………………………… baada ya kufanya ukaguzi katika eneo husika ili kutathimini athari za mazingira.

Kutokana na uzingatiaji wa athari za Mazingira mchimbaji anaruhusiwa kuchimba madini ya ujenzi katika eneo hilo kwa muda wa miezi kumi na mbili tu. Mwombaji analazimika kuomba tena kibali baada ya muda huo kuisha na ukaguzi utafanyika tena.

<u>TAMKO LA MWOMBAJI:</u>

MIMI………………………………………………………nipo tayari kufuata masharti ya kibali hiki cha Uchimbaji wa Madini ya Ujenzi ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba kwa lengo la kutunza na kuhifadhi mazingira. Nathibitisha kwa hiari yangu nimeelewa vema masharti ya kibali hiki.

Jina: ……………………………………… Saini ………………….. Tarehe …………………

*<u>KWA MATUMIZI YA OFISITU:</u>*

Mwombaji amelipia Shilingi ……………. tarehe……….mwezi………….Mwaka…………..

(Ambatanisha stakabadhi ya malipo na fomu hii)

*Tangazo La Serikali Na. 909 (Linaendelea))*

Jina la Afisa aliyetoa kibali……………………… Saini …………… Tarehe ……………….

Muhuri: ………………………………………….

---

JEDWALI LA PILI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 8(1))*

USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Namba | Aina ya Madini | Ujazo au Tani | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mawe | Tani 3 –Tani 7 | 3,000/= kwa tripu |
| 2. | Moramu | Tani 3 –Tani 7 | 2,000/= kwa tripu |
| 3. | Mchanga | Tani 3 –Tani 7 | 2,000/= kwa tripu |
| 4. | Kokoto | Tani 3 –Tani 7 | 5,000/= kwa tripu |
| 5. | Mawe au Moramu au Mchanga au Kokoto | Zaidi ya Tani 7 | 3% ya Bei ya Madini husika |

---

JEDWALI LA TATU

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 16)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi; ……………………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya; ……………………………………..……. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, kwamba mnamo tarehe;…… ya Mwezi;……. Mwaka; ………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya…….. ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ya Mwaka 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU:

Leo tarehe;…....... ya Mwezi;………… Mwaka;…………..
Jina;………………………………..…………………….
Saini;………………………..……………………………

MBELE YANGU :
Jina;…………………………..……...……………………
Wadhifa;…………………………………………….....…
Saini;…………………………………………………………
Tarehe;……………………………………………………….

*Tangazo La Serikali Na. 909 (Linaendelea))*

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya Mlimba imegongwa kwenye sheria Ndogo hii kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani Halmshauri ya Wilaya ya Mlimba uliofanyika Tarehe 27 Mwezi Oktoba Mwaka 2021 na Kushudiwa na Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya :-

ENG. STEPHANO B. KALIWA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba*

INNOCENT SIMON MWANGASA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba*

NAKUBALI,

Dodoma,
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*